

TANGAZO KUHUSU ZOEZI LA UBORESHAJI WA DAFTARI

AFISA MWANDIKISHAJI WA JIMBO LA SONGEA MJINI ANAPENDA KUWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUWA TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI IPO KATIKA HATUA YA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA, AMBAPO KWA MANISPAA YA SONGEA ZOEZI LA UBORESHAJI LITAFANYIKA KWA MUDA WA SIKU SABA (7) KUENZIA TAREHE 12/01/2025 HADI 18/01/2025 SAA 2:00 ASUBUHI HADI SAA 12:00 JIONI KATIKA VITUO VYA UANDIKISHAJI VILIVYOPO KWENYE KILA MTAU KATIKA KATA ZOTE ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA JIMBO LA SONGEA MJINI. UBORESHAJI UTAHUSISHA:

1. KUANDIKISHA WAPIGA KURA WAPYA WALIOTIMIZA UMRI WA MIAKA 18 NA KUENDELEA AMBAO HAWAJAWAHI KUANDIKISHWA;
2. KUANDIKISHA WATAKAOTIMIZA UMRI WA MIAKA 18 KABLA AU IFIKAPO SIKU YA UCHAGUZI MKUU MWEZI OKTOBA 2025;
3. KUANDIKISHA WATU WENYE SIFA AMBAO HAWAKUJIANDIKISHA MWAKA 2020;
4. KUHAMISHA TAARIFA ZA WAPIGA KURA WALIOJIANDIKISHA AWALI NA WAMEHAMA MAKAZI KUTOKA KATA AU JIMBO JINGINE;
5. KUREKEBISHA TAARIFA ZILIZOKOSEWA WAKATI WA UANDIKISHAJI MFANO MAJINA;
6. KUTOA KADI MPYA KWA WAPIGA KURA WALIOPOTEZA AU KADI ZAO KU HARIBIKA
7. KUONDOA AU KUFUTA TAARIFA ZA WAPIGA KURA WALIOPOTEZA SIFA IKIWEMO WALIOFARIKI